



OFISI YA RAIS - IKULU



**MPANGO WA KURASIMISHA  
RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA  
(M K U R A B I T A)**

**Uwezeshaji wa Wamiliki Wa Hati Za  
Hakimiliki Za Kimila Kupata Mikopo Kutoka  
Kwenye Taasisi Za Kifedha**

Imeandaliwa na Menejimenti ya MKURABITA

Mei, 2018

Kitalu na. 20, Ocean Road | S.L.P 7975 | DSM|Tanzania

Simu: +255 22 2126250/3 | Nukushi: +255 22 2126252 | Barua-pepe: [info@mkurabita.go.tz](mailto:info@mkurabita.go.tz)

Tovuti: [www.mkurabita.go.tz](http://www.mkurabita.go.tz)

## **YALIYOMO**

1.0 UTANGULIZI .....	3
2.0 MBINU ZA UTOAJI MAFUNZO.....	4
2.1 Mafunzo ya wakufunzi.....	4
2.2 Miongozo ya Mafunzo.....	5
2.3 Mafunzo kwa wakulima .....	5
2.3.1 Mada za mafunzo kwa wakulima .....	5
2.3.2 Huduma za Kibenki.....	6
2.3.3 Utunzaji wa kumbukumbu za biashara kwa wakulima binafsi: .....	6
2.3.4 Tathmini ya mahitaji ya Pembejeo za Kilimo .....	7
2.3.5 Uandaaji wa Mpango wa Biashara:.....	7
2.3.6 Kufanya Tathmini ya Mashamba:.....	8
2.3.7 Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Mazao .....	8
2.4 Mafunzo kwa Viongozi wa Vyama vya Wakulima/ Vyama vya Ushirika .....	9
Mada za Mafunzo kwa Viongozi wa Vyama vya Wakulima: .....	9
3.0 WAJIBU WA WASHIRIKA WA UTOAJI MAFUNZO .....	9
3.1 Taasisi za Kifedha .....	10
3.2 Mamlaka za Serikali za Mitaa .....	10
3.3 Viongozi wa Vyama vya Wakulima na Vyama vya Ushirika .....	10
3.4 Kitengo cha Usimamizi wa Mpango wa MKURABITA .....	10
4.0 HALMASHAURI ZILIZOFIKIWA KWA AJILI YA MAFUNZO.....	11
5.0 MAFANIKIO .....	12
5.1 Wakulima kuunganishwa na Taasisi za fedha, Bima za Afya na Mifuko ya Kijamii .....	12
5.2 Udhagini wa Vyama vya Ushirika kwa wakulima.....	14
6.0 CHANGAMOTO.....	15

7.0 MIPANGO WA BAADAYE .....	15
------------------------------	----

## 1.0 UTANGULIZI

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ulianza utekelezaji wa Awamu ya Mapendekezo ya Maboresho mwezi Julai 2008. Lengo kuu lilikuwa ni kusambaza mapendekezo ya maboresho katika Wizara za kisekta Tanzania Bara na Zanzibar. Hata hivyo, ili kufanya majaribio ya baadhi ya mapendekezo ya maboresho, urasimishaji wa rasilimali na biashara ulipangwa kufanya sambamba na kuwawezesha wananchi kiuchumi katika Upatikanaji wa Mitaji na Utawala Bora.

Mwaka wa fedha 2011/2012, MKURABITA ilianza utekelezaji wa Awamu ya nne ambayo ni kujengea uwezo wananchi ili waweze kupata mitaji. MKURABITA ilianza kuwajengea uwezo wamiliki wa Hati za Hakimiliki za Kimila, ili waweze kuzitumia kupata mikopo kutoka taasisi za fedh. MKURABITA ilianza kuwajengea uwezo wamiliki wa mashamba ya chai, kwa kushirikiana na Bodi ya Chai Tanzania na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai. Utekelezaji ulianza kwa kufanya uhakiki wa mashamba yanayomilikiwa na wakulima wa chai katika Wilaya za Njombe na Mufindi. Lengo kuu lilikuwa ni kuwajengea uwezo wakulima wa chai ili waweze kutumia ardhi zao zilizorasmishwa kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha. Wakulima walipewa mafunzo mbalimbali ambayo yalilenga kuwawezesha kutumia Hati za Hakimiliki za Kimila katika kupata mikopo kwenye taasisi za fedha.

MKURABITA iliandaa miongozo wa mafunzo yenye mada ambazo zilizingatia vipengele muhimu ambavyo vinahitajika na Taasisi za fedha ili mkulima aweze kupata mkopo.



*Picha na. 1: Shamba la Chai katika Halmashauri ya Mji wa Njombe, Kijiji cha Kitulila.*

Vipengele vya mafunzo vilihusisha huduma za kibenki kwa wakulima binafsi na vyama vya wakulima, utunzaji wa kumbukumbu za biashara kwa wakulima na vyama vya wakulima, namna ya kufanya tathmini ya mahitaji ya pembejeo za kilimo, uandaaji wa mipango ya biashara, kufanya tathmini ya mashamba ya wakulima, sheria na kanuni zinazosimamia sekta ya chai na usimamizi wa vyama vya wakulima.

Miongozo ilibainisha pia wakufunzi ambao walitoka katika Taasisi mbalimbali kulingana na mada za mafunzo kama ifuatavyo;

- i. Elimu ya Huduma za kibenki ilitolewa na Benki za CRDB au NMB kutegemea na upatikanaji wa benki hizo katika eneo husika;
- ii. Elimu ya utunzaji wa kumbukumbu za biashara kwa wakulima ilitolewa na MKURABITA;
- iii. Tathmini ya mahitaji ya pembejeo za kilimo ilitolewa na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai;
- iv. Uandaaji wa mipango ya biashara ilitolewa na MKURABITA;
- v. Tathmini ya mashamba ya chai ilitolewa na Mthamini wa Halmashauri ya Wilaya;
- vi. Sheria na Kanuni zinazosimamia sekta ya chai ilitolewa na Bodi ya Chai Tanzania;
- vii. Usimamizi wa vyama vya wakulima ilitolewa na Afisa wa Vyama vya Ushirika wa Halmashauri ya Wilaya au Afisa Maendeleo ya Jamii.

## **2.0 MBINU ZA UTOAJI MAFUNZO**

MKURABITA inatumia mbinu ya kuandaa wakufunzi ambao wanapatikana kutoka katika Taasisi mbalimbali ambazo ni Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Kifedha (hasa benki ya CRDB na NMB), Vyama vya Wakulima, Vyama vya Ushirika, Bodi ya Chai Tanzania (TBT), Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA), Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na sekta binafsi. Mafunzo kwa wakulima hutolewa kwa ushirikiano wa wadau wote hawa ili kuwezesha mafunzo kuwa endelevu. Aidha, mafunzo haya hufanywa sambamba na utekelezaji wa mipango ya jamii. Sehemu hii inaelezea miongozo ya mafunzo kwa watoa mafunzo, wawezeshaji pamoja na vipengele vya mafunzo.

### **2.1 Mafunzo ya wakufunzi**

MKURABITA ilibainisha na kutoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wanaofanya kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na wadau wengine ili wawe wakufunzi na waweze kuendelea kutoa mafunzo kwa wakulima pale

inapohitajika, hasa baada ya MKURABITA kukamilisha mafunzo kwenye eneo moja la Halmashauri. Wakufunzi hawa hujifunza mada zote na baada ya mafunzo wanakuwa tayari kutoa mafunzo kwa wakulima

## **2.2 Miongozo ya Mafunzo**

Lengo kuu la miongozo ya mafunzo ni kuhakikisha kwamba, mafunzo yote yanayotolewa kwa viwango vya aina moja, sahihi na yanalenga kutimiza lengo la kuwawezesha wakulima kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha. Miongozo huandaliwa pia kuwaongoza wakufunzi waweze kuzingatia vipengele vyote na utoaji wa mada uweze kufanana kutoka Hamahsauri moja hadi nyingine.

Mafunzo yamegawanyika katika sehemu mbili kama ifuatavyo:

- i. Mafunzo kwa wakulima binafsi; na
- ii. Mafunzo kwa viongozi wa vyama vya wakulima.

## **2.3 Mafunzo kwa wakulima**

Wakulima binafsi huchaguliwa kushiriki katika mafunzo kulingana na ukubwa wa mashamba yao. Uchaguzi unazingatia kiwango cha ekari ambazo mkulima anaweza kulima kwa faida. Ili kuweza kurudisha gharama za kilimo na kupata faida, mkulima wa chai anatakiwa kulima angalau ekari 2.5. Hivyo, wakulima wenye mashamba yenye ukubwa wa zaidi ya ekari 2.5 ndio huchaguliwa kushiriki katika mafunzo. Kwa wakulima wa korosho, mashamba yenye ukubwa wa zaidi ya ekari 10 yanao uwezo wa kutoa faida kwa mkulima. Hivyo, mafunzo yalitolewa kwa wakulima wa korosho wenye mashamba yenye ukubwa wa zaidi ya ekari 10.

### **2.3.1 Mada za mafunzo kwa wakulima**

Mada zinazofundishwa ni zile ambazo zimelenga kuwasaidia wakulima kupata mitaji. Mada hizo ni kama ifautavyo:-

- i. Huduma za kibenki kwa wakulima binafsi;
- ii. Utunzaji wa kumbukumbu za biashara kwa wakulima binafsi;
- iii. Ufanyaji wa tathmini ya pembejeo za kilimo kwa wakulima binafsi;
- iv. Uandaaji wa mpango wa biashara kwa wakulima;
- v. Ufanyaji tathmini za mashamba binafsi ya chai;
- vi. Sheria na kanuni zinazosimamia sekta ya mazao.

Lengo kuu la mafunzo haya ni kuwawezesha wakulima binafsi kuwa na uwezo wa kupata mitaji kutoka kwenye taasisi za kifedha.

### 2.3.2 Huduma za Kibenki

Mada hii ya mafunzo hutolewa na benki ya CRDB au NMB kulingana na uwepo wa matawi ya benki hizo katika eneo husika.

**Lengo kuu:** Mafunzo ya huduma za kibenki hutolewa ili kujenga uelewa wa huduma zote zinazotolewa na taasisi za kifedha na hatimaye, mkulima aweze kuwa mteja wa taasisi hizo na kupata huduma zote ikiwa ni pamoja na uwekaji wa akiba, mikopo na utumaji wa fedha. Wakulima pia huelezewa kuhusu mambo ya kufanya na kutofanya katika kujenga uhusiano na taasisi za kifedha.

**Muda wa mafunzo wa Mada:** Mafunzo hutolewa kwa siku moja kwa muda usiozidi masaa mawili.

**Mada ndogo:** Mafunzo hutolewa kwa kufuata mtiririko wa mada ndogo zifuatazo:-

- i. Utangulizi wa mada;
- ii. Huduma zinazotolewa na benki;
- iii. Aina za wateja wa benki;
- iv. Vigezo na masharti ya mikopo;
- v. Majukumu ya benki kwa wateja.

### 2.3.3 Utunzaji wa kumbukumbu za biashara kwa wakulima binafsi:

Mada hii ya mafunzo hutolewa na watalaam kutoka MKURABITA,

**Lengo kuu:** Mafunzo hutolewa ili kuwawezesha wakulima kuweka kumbukumbu rahisi za biashara na kuendesha kilimo cha biashara katika mashamba yao. Mada inawezesha kutimiza vigezo vya kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha, kuelewa kama shughuli zao za kilimo zinazalisha faida au hasara na kuweza kupanga shughuli zao za kilimo kwa ufanisi.

**Muda wa mafunzo wa Mada:** Saa moja ikiwa ni pamoja na majadiliano na maswali.

**Mada ndogo:** Mada imegawanywa katika mada ndogo nane (8) kama ifuatavyo:-

- i. Utangulizi wa mada;
- ii. Umuhimu wa kutunza kumbukumbu za biashara;
- iii. Aina za kumbukumbu;
- iv. Ripoti za mauzo;
- v. Ripoti za gharama;

- vi. Ripoti za wadaiwa;
- vii. Ripoti za wadai;
- viii. Ripoti za mapato na matumizi.

#### **2.3.4 Tathmini ya mahitaji ya Pembejeo za Kilimo**

Mada hii ya mafunzo, hutolewa na Maafisa wa Maendeleo ya Kilimo kutoka katika halmashauri za wilaya pamoja na taasisi ambazo husimamia mazao ya biashara. Mfano, wakati wa mafunzo ya wakulima wa chai, Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA) amekuwa mdau muhimu katika kutoa mafunzo.

**Lengo Kuu:** Kuwawezesha wakulima kufanya tathmini na makadirio ya mahitaji ya pembejeo mbalimbali za kilimo kama inavyofanywa na wakulima wa kibiashara ili kukuza ufanisi.

**Muda wa Mafunzo wa mada:** Mafunzo haya huchukua muda usiozidi saa moja ikiwa ni pamoja na maswali na majadiliano

**Mada ndogo:**

- i. Utangulizi wa mada;
- ii. Makadirio ya mahitaji ya mbolea;
- iii. Virutubisho muhimu;
- iv. Aina za mbolea;
- v. Aina za dawa za kuua magugu.

#### **2.3.5 Uandaaji wa Mpango wa Biashara:**

Mada hii ya mafunzo hutolewa na watalaam kutoka MKURABITA.

**Lengo Kuu:** Kuwawezesha wakulima kuelewa mahitaji ya Mpango wa Biashara na kuweza kutimiza vigezo na masharti ya kupata mikopo. Mafunzo haya huwasaidia wakulima kuelewa umuhimu wa kuwa na Mpango wa Biashara ambao utasaidia Taasisi za Fedha kufanya Tathimini ya kilimo chao.

**Muda wa Mafunzo :** Mada huchukua zaidi ya saa moja.

**Mada ndogo:** Mada imegawanywa katika mada ndogo tano (5) kama ifuatavyo;

- i. Maana ya Mpango wa Biashara;
- ii. Umuhimu wa Mpango wa Biashara;
- iii. Kufanya makadirio ya uzalishaji;
- iv. Kufanya Mipango ya mauzo na gharama za uzalishaji;

- v. Vipengele vilivyopo katika Mpango wa Biashara;

### **2.3.6 Kufanya Tathmini ya Mashamba:**

Mada hii ya mafunzo hutolewa na Mthamini wa Halmashauri ya Wilaya ambayo wakulima wake wanapewa mafunzo kwa wakati huo.

**Lengo Kuu:** Kuwawezesha wakulima kuelewa vigezo vyta kufanya tathmini ya mashamba yao, ili waweze kuboresha huduma za kilimo na kuongeza thamani ya mashamba yao. Aidha, mada inamsadia mkulima kujua thamani ya shamba lake.

**Muda wa Mafunzo wa Mada:** Muda wa mafunzo hauzidi saa moja ikiwa ni pamoja na majadiliano.

**Mada ndogo:** Mada imegawanywa katika mada ndogo sita (6) ambazo ni:

- i. Takwimu katika sekta ya mazao mbalimbali;
- ii. Taarifa muhimu kwa Mfanya Tathmini;
- iii. Vigezo muhimu ambavyo hutumika katika kufanya tathmini za mashamba;
- iv. Mbinu tofauti zinazotumika kufanya tathmini za mashamba;
- v. Masuala yanayoathiri ufanyaji wa tathmini za mashamba;
- vi. Jinsi benki zinavyofanya tathmini ya thamani ya shamba litakalotumika kama dhamana.

### **2.3.7 Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Mazao**

Mada hii ya mafunzo hutolewa na Bodi za Usimamizi wa Mazao ya Biashara ambazo ni Bodi ya Chai, Bodi ya Kahawa, Bodi ya Korosho na nyingine kutegemea wakulima wanalima zao gani.

**Lengo Kuu:** Kuwawezesha wakulima kuelewa sheria na kanuni zinazosimamia sekta ya zao ambalo wanalima, ili uzalishaji na uuzaaji wa mazao yao uweze kuzingatia sheria na kanuni husika.

**Muda wa Mafunzo:** Mada hii hutolewa kwa muda usiozidi saa mbili ikiwa ni pamoja na maswali na majadiliano.

**Mada ndogo:**

- i. Utangulizi wa Mada;
- ii. Kuelezea maana ya maneno mbalimbali yanayotumika katika tasnia ya zao husika;
- iii. Malipo kutokana na mauzo ya mazao;
- iv. Ubora, kupima uzito na ukaguzi wa mazao;
- v. Ukaguzi wa uzito na vipimo;

- vi. Kilimo cha mkataba;
- vii. Makubalino katika mauzo ya mazao;
- viii. Majukumu ya mnunuzi wa mazo;
- ix. Utaratibu wa kuweka bei elekezi

#### **2.4 Mafunzo kwa Viongozi wa Vyama vya Wakulima/ Vyama vya Ushirika**

Viongozi hawa ni wajumbe wa kamati za utendaji za vyama vya wakulima na vyama vya ushirika. Mafunzo yanalenga kuwajengea uwezo ili waweze kuhudumia wanachama wao ambao ni wakulima.

**Lengo Kuu:** Mafunzo haya yana lengo la kuwaelewesha viongozi wa vyama, kuhusu majukumu yao kama wadhamini katika mikopo ya wakulima inayodhaminiwa na vyama vya wakulima. Taasisi za kifedha hupendelea zaidi kujihusisha na vyama vya wakulima kuliko mkulima mmoja mmoja. Kuwajengea uwezo viongozi wa vyama vya wakulima husaidia kuleta ufanisi na kuona thamani ya vyama vya wakulima.

#### **Mada za Mafunzo kwa Viongozi wa Vyama vya Wakulima:**

- i. Huduma za kibenki kwa vyama vya wakulima;
- ii. Utunzaji wa kumbukumbu za biashara kwa vyama vya wakulima;
- iii. Kufanya tathmini ya mahitaji ya pembejeo za kilimo;
- iv. Uandaaji wa mpango wa bishara kwa ajili ya chama cha wakulima;
- v. Ufanyaji wa tathmini ya rasilimali kwa ajili ya kuweka dhamana;
- vi. Majukumu ya uongozi katika chama cha wakulima.

Mada ndogo zinazofundishwa wakati wa mafunzo ya viongozi wa vyama hazina tofauti na mada ndogo za utunzaji wa kumbukumbu za biashara. Viongozi wa vyama hufundishwa utunzaji wa kumbukumbu za vyama vyao kwa kuzingatia sheria na kanuni za vyama vya ushirika nchini

#### **3.0 WAJIBU WA WASHIRIKA WA UTOAJI MAFUNZO**

Utoaji wa mafunzo kwa wakulima, unahusisha wadau mbalimbali ili kuwapa wakulima hali halisi ya utendaji pamoja na kuwapa taarifa zitokanazo na uzoefu wa wadau mbalimbali. Kutokana na hilo, Wakufunzi hupatikana katika maeneo ambapo mafunzo hufanyika, kama vile Maafisa wa Maendeleo ya Kilimo na Ufugaji (baadhi hutoka katika ngazi ya kata na ngazi ya kijiji), ngazi ya halmashauri ya wilaya, Taasisi za Kifedha zinazotarajiwa kutoa huduma kwa wakulima, Maafisa wa Bodi za Mazao

walio katika ngazi ya jamii ili waweze kutoa elimu kwa wakulima, Maafisa wa Maendeleo ya Vyama vya Ushirika katika ngazi ya Serikali za Mitaa na sekta binafsi katika ngazi ya jamii au makao makuu ya wilaya. Mfumo huu husaidia utoaji wa huduma endelevu kwa wakulima baada ya mafunzo kukamilika.

### **3.1 Taasisi za Kifedha**

Taasisi za kifedha hazina mazoea ya kutafuta wateja kwa kuwafata walipo, husubiria wateja waende katika ofisi zao kupata huduma. Mafunzo haya hutoa fursa kwa taasisi za kifedha kuwafahamu wakulima na mahitaji yao na pia hutoa fursa ya kuanzisha mahusiano na wateja wapya. Kwa mfano, benki ya NMB na CRDB huanza kwenda katika vijiji ambavyo wakulima wamepewa mafunzo kwa ajili ya kufungua akaunti za benki kwa wateja wapya.

### **3.2 Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Watalaam kutoka Serikali za Mitaa wanaoshiriki katika mafunzo, hubaki katika Halmashauri kuendelea na utoaji wa huduma baada ya kumalizika kwa mafunzo ya MKURABITA. Maafisa wa Maendeleo ya Kilimo na Mifugo, Wathmini, Maafisa Ardhi, na Maafisa wa Maendeleo ya Jamii huanza kushiriki kikamilifu katika kutoa mafunzo kwa vijiji vingine ambavyo vimefanyiwa urasimishaji katika Halmashauri zao.

### **3.3 Viongozi wa Vyama vya Wakulima na Vyama vya Ushirika**

Viongozi wa vyama vya wakulima au vyama vya ushirika, wanatarajiwu kuwa wadhamini wa mikopo ya wakulima wadogo kwenye taasisi za kifedha. Mafunzo haya huwapa viongozi hao ujuzi wa kutathmini mahitaji ya wakulima kuhusu pembejeo za kilimo, masuala ya uongozi, uandaaji wa mipango ya biashara kwa vyama vyao na utunzaji wa kumbukumbu sahihi za biashara.

### **3.4 Kitengo cha Usimamizi wa Mpango wa MKURABITA**

Jukumu la MKURABITA ni kujenga uwezo kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ili waweze kutoa huduma endelevu za kuwawezesha wakulima kupata huduma za mikopo zinazotolewa na taasisi za kifedha. MKURABITA huandaa miongozo na kuratibu mafunzo haya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

#### **4.0 HALMASHAURI ZILIZOFIKIWA KWA AJILI YA MAFUNZO**

Katika kipindi cha mwaka 2011/12 Hadi Mei, 2018, MKURABITA imendaa na kuratibu mafunzo kufanyika katika halmashauri za wilaya 21 za Tanzania Bara. Wakulima 2912 wamepata mafunzo ya kutumia Haki za Hakimiliki za Kimila. Aidha, Viongozi 555 wa Vyama vya Ushirika vya Wakulima wamepata mafunzo ya usimamizi na uendeshaji ili viweze kuwadhamini wakulima kupata mikopo kutoka Taasisi za fedha.

Kwa muhtasari, halmashauri zilizofikiwa kwa ajili ya mafunzo ya kuwawezesha wakulima kutumia Hati za Hakimiliki za Kimila, yameoneshwa kwenye jedwali namba 1.

*Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Mafunzo ya Uwezeshaji*

Na.	Halmashauri ya Wilaya	Wakulima waliopewa mafunzo	Viongozi waliopewa mafunzo
1	Mji wa Njombe	34	12
2	Wilaya ya Njombe	115	32
3	Mufindi	144	20
4	Rungwe	36	14
5	Mtwara	107	18
6	Tandahimba	100	27
7	Manyoni	172	18
8	Meru	127	25
9	Mwanga	124	22
10	Sumbawanga	128	20
11	Kalambo	46	9
12	Mbinga	90	34
13	Kilombero(Idete)	206	23
	Kilombero(miwa)	142	32
14	Kilosa(Miwa)	164	21
15	Karagwe	193	19
16	Ludewa	66	12
17	Misungwi	200	20
18	Mbarali	109	28
19	Korogwe	220	80
20	Mpwapwa	182	36

21	Serengeti	207	33
	Jumla	2,912	555



*Picha na. 2.: Mshiriki wa mafunzo akitoa mchango wake katika kipindi cha majadiliano wakati wa mafunzo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara mwaka 2014*

## 5.0 MAFANIKIO

MKURABITA imetoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa wakulima binafsi 2912 na viongozi 555 wa vyama vya wakulima katika Halmashauri za Wilaya 21 za Njombe Mji, Njombe, Mufindi, Mtwara, Tandahimba, Manyoni, Rungwe, Meru, Mwanga, Sumbawanga, Kalambo, Mbinga, Kilombero, Kilosa, Karagwe, Ludewa, Misungwi, Mbarali, Korogwe, Mpwapwa na Serengeti.

Mafunzo ya kujenga uwezo katika halmasahuri, yalitolewa kwa wakulima waliokidhi vigezo vya kuwa na mashamba ya ukubwa unaoleta faida na tija, ambayo yamesharasimishwa na wamiliki kupatiwa Hati za Hakimiliki za Kimila katika vijiji vilivyofanya urasimishaji.

### 5.1 Wakulima kuunganishwa na Taasisi za fedha, Bima za Afya na Mifuko ya Kijamii

Katika kuwajengea uwezo wakulima waliorasimiza ardhi zao na kupata Hati za Hakimiliki za Kimila, wakulima 2,912 na viongozi wa vyama vya wakulima 555 kutoka katika Halmashauri za wilaya 21, wamepata mafunzo ya kutumia hati za ardhi yao na kuunganishwa na taasisi za fedha zikiwemo CRDB, NMB na TPB ili kupata mitaji na kufanya kilimo chenye tija.

Aidha, katika mafunzo hayo Halmashauri ya Mbinga; wakulima 18, halmashauri ya kilombero; wakulima 56, Kilosa; wakulima 29, Karagwe; wakulima 15, Misungwi; wakulima 70, Mpwapwa; wakulima 28, na Serengeti; wakulima 42, ndio walioweza kutumia fursa ya kufungua akaunti katika benki za NMB na CRDB wakati wa Mafunzo.

Pia katika Halmasahuri ya Mbinga, wakulima saba (7) walijiunga na bima ya afya ya CHIF na 12 wakajiunga na mfuko wa jamii wa NSSF; Halmashauri ya Kilombero wakulima tisa walijiunga na mfuko wa NSSF wakati wa Mafunzo.

Mafunzo yamewezesha, Wakulima **531** wenye Hatimiliki za kimila kutumia hati kama dhamana na kupata mikopo yenyeye thamani ya shilingi bilioni **5.46**. kutoka katika Taasisi za fedha. Mikopo hii imepatikana kutoka katika Taasisi za Fedha, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na Vyama vya Ushirika na Mifuko ya Pembejeo.



*Picha na. 3: Wakulima wa kijiji cha Robanda wilayani Serengeti wakifungua akaunti katika benki za CRDB na NMB kijijini kwa wakati wa Mafunzo ya kujengewa uwezo, mwaka 2018*

Jedwali namba 2 linaonesha Idadi ya wakulima walionufaika na Mikopo kwa kutumia Hati ya Hakimiliki ya kimila kama Dhamana. Aidha, jedwali limeainisha Taasisi ambazo zimetoa mikopo kwa wakulima

*Jedwali Na.2: Idadi ya wakulima walionufaika na Mikopo kwa kutumia Hati ya Hakimiliki ya kimila kama Dhamana*

1	WILAYA	IDADI YA VIJIJI	IDADI YA WANUFAIKA	AINA YA KILIMO	KIASI CHA MKOPO	TAASISI ZILIZOKOPESHA
2	MAKETE	5	20	MATUNDA	50,000,000.00	NMB & POST BANK
3	MVOMERO	4	5	MPUNGA	154,000,000.00	NMB & SACCOS
4	MUFINDI	20	10	CHAI	100,000,000.00	CRDB
5	MBINGA	15	15	KAHAWA	500,000,000.00	CRDB
6	TANDAHIMBA	1	1	KOROSHO	40,000,000.00	NMB
7	MANYONI	3	8	ALIZETI	181,500,000.00	PSPF& NMB
8	MTWARA	4	8	KOROSHO	120,000,000.00	PSPF
9	KOROGWE	2	21	SHAMBA LA MITIKI	521,000,000.00	CRDB
10	MOSHI	1	5	KAHAWA	50,000,000.00	NMB
11	MBARALI	2	40	MPUNGA	600,000,000.00	CRDB & NMB
12	MAGU	1	1	MPUNGA	13,000,000.00	CRDB
13	KITETO	3	43	MAHINDI	125,700,000.00	FINCA & NMB
14	MPWAPWA	2	21	MBOGAMBOGA	100,600,000.00	CRDB & FINCA
15	MISUNGWI	3	21	MATIKITI MAJI	530,000,000.00	NSSF & SUMA JKT
16	HANDENI	2	2	MAHINDI	10,000,000.00	AGITF
17	LUDEWA	1	2	MAHINDI	80,000,000.00	NMB
	KILOMBERO	2	160	MIWA	406,000,000.00	TADB
18	KILOMBERO	1	1	MIWA	150,000,000.00	CRDB
19	SUMBAWANGA	11	26	MAHINDI	650,000,000.00	PSPF
20	NJOMBE DC	3	104	MITI YA MBAO	522,850,000.00	NYOMB SACCOS
	KILOSA	4	17	MIWA	556,708,600.00	TADB
	JUMLA	90	531		5,625,358,600.00	

## 5.2 Udhamini wa Vyama vya Ushirika kwa wakulima

Miongoni mwa malengo ya mafunzo ilikuwa ni kuwezesha vyama vya wakulima kudhamini wakulima kupata mikopo kutoka Taasisi za Fedha. Hadi kufikia Mei, 2018

Chama cha Wakulima wa Chai Igominyi, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kimedhamini mkopo wa Shilingi Milion 625.9 kwa wakulima wa chai.

## 6.0 CHANGAMOTO

Uwezeshaji wa wakulima kwa njia ya kutoa mafunzo ni dhana mpya kwa wadau wengi ambao wanashiriki. Kwa upande wa wakulima, wao hawajazoea kupata mafunzo ya darasani, kwa taasisi za kifedha wao hawajazoea kuwafuata wakulima walipo ili kuwapa huduma, kwa watalaam wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa wao pia hawana uzoefu na aina hii ya mafunzo. Kuna changamoto kadhaa zilizojitokeza katika mchakato huu: -

1. Kutokana na kutozoea kukaa darasani, muda ambao wakulima wanautumia darasani ni mrefu kutokana na mada mbalimbali ambazo ni muhimu kuwepo kwenye mafunzo hayo. Ili kutatua changamoto hii, Mahitaji ya wakulima yamebainishwa ili yatumike katika kufanya mapitio ya mada;
2. Baadhi ya wakulima hawajui kusoma na kuandika na baadhi yao ni wazee sana, hivyo hawawezi kukaa darasani kwa muda mrefu. Katika kutatua changamoto hii, wanandugu walioko karibu na wakulima wasiojua kusoma pamoja na wazee, watashauriwa kuwasaidia pale watakapohitaji kusaidiwa.
3. Ugumu katika kubainisha wafanyakazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao wanaweza kutoa huduma hizi na ufuatiliaji wa utendaji wao. Ili kutatua changamoto hii, MKURABITA kwa kushirikiana na Halmashauri watabainisha wafanyakazi husika;
4. Baadhi ya mada ambazo ni muhimu zimeonekana kuwa ngumu kuelewka. Mfano; uandaaji wa Mpango wa Biashara na Utunzaji wa kumbukumbu za biashara. Ili kutatua changamoto hii, wataalamu husika wa Halmashauri wataendelea kuwasaidia wananchi hata baada ya mafunzo ili waweze kupata uelewa.

## 7.0 MIPANGO WA BAADYE

MKURABITA itaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na wadau wengine, ili kuhakikisha kuwa walengwa wa Mpango wa mafunzo wanajengewa uwezo wa kutumia Hati za Hakimiliki za Kimila, ili kupata mitaji ya kuendesha shughuli zao.